KWAYA YA MTAKATIFU KIZITO
PAROKIA YA MWENYEHERI ANUARITE MAKUBURI
+255742000089|+255713975788
kmkmakuburi
www.kmkmakuburi.co.tz
stkizitochoir@gmail.com

KIMEELEWEKA-B. MUKASA

Kiitikio

Kilichomfanya Baba amtoe mwanaye wa pekee, kilichomfanya Mwana akubali kufa kifo cha aibu, Kimefafanuliwa, kimeeleweka leo kimefafanuliwa kimeeleweka kimeeleweka

Mashairi

1. Alimuona mwanadamu, anaanguka kuzimu, Akaja kumuinua, akakibugia kifo
   Akashuka nacho, kuzimu kisha, akakiacha huko

2. Alijua udanganyifu wa Ibilisi mzushi, Akaja kuuharibu na kufunua ukweli
   Kuzigaragaza, hila za mwovu, na kumuaibisha

3. Alimpenda mwanadamu, akampenda upeo, Kajifanananisha naye bali
   hakutenda dhambi, Akamuinua, kiumbe huyu, kampandisha hadhi

Hitimisho

Amevishinda vita vya imani, Mshindi! Amevaa utukufu na enzi mwokozi!
Ae katangaza mlango wa Mbingu u wazi! Ae na urithi wa utawala,
Kafufuka, kama alivyosema Yesu, Amefufuka ameyashinda mauti
Kafufuka, kama alivyosema Yesu, Amefufuka ameyashinda mauti
Kaivunja milango yote ya Kuzimu, ameivunja ameyashinda mauti
Kafufuka, kama alivyosema Yesu, Amefufuka ameyashinda mauti
Kaonesha, ya kwamba inawezekana, ameonesha, ameyashinda mauti
Kafufuka, kama alivyosema Yesu, Amefufuka ameyashinda mauti
Kwa hiyo tuimbe Aleluya kwa shangwe kuu, kwa hiyo tuimbe aleluya kwani
Bwana ameyashinda mauti. Ameyashinda mauti, Ameyashinda mauti,
Ame ame ame ame ameyashinda mauti